



**USAID**  
KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI



Kaimu Balozi, Inmi Patterson, akisalimiana na Mhudumu wa ngazi ya Jamii, Joyce Paulo, wakati wa hafla ambayo mradi wa Boresha Afya-Sothern Zone ulipoahidhisha ushirikiano baina ya Serikali ya Marekani na Serikali ya Tanzania na Asasi za Kiraia katika kuboresha utoaji wa huduma za afya.

Picha: Stephen Mhando (Deloitte)

## TANZANIA

## BORESHA AFYA – SOUTHERN ZONE

Mradi wa USAID Boresha Afya unaboresha Afya – Mradi wa Boresha Afya Southern zone unafanya kazi kushughulikia mapungufu ya huduma za afya katika maeneo yote ya mikoa ya Iringa, Njombe, Morogoro, Lindi, Mtwara, na Ruvuma. Mradi huu hutumia njia inayolenga mahitaji ya mteja katika kutoa huduma kwenye maeneo yenye kiwango cha juu cha VVU, Kifua Kikuu, Malaria, na maeneo yenye uhitaji mkubwa wa huduma za uzazi wa mpango na huduma za afya ya mama na mtoto. Mradi huu unasaidia pia ujumuishaji wa huduma mbali mbali za afya ndani ya vituo, na hivyo kuboresha ufanisi, kuongeza matumizi sahihi ya rasilimali, na kuhakikisha wateja wanapata huduma mbali mbali kutoka eneo moja.

VVU, Malaria, na kifua kikuu (TB) ni mionganini mwa sababu zinazoongoza katika kusababisha maradhi (yaani ugonjwa au ulemavu) na vifo nchini Tanzania. Hii inazidishwa na ukosefu wa huduma za afya ya mama, mtoto na familia kwa raia wa Tanzania, haswa kwa wanawake na vijana wa rika balehe. Ukosefu wa huduma bora za afya jumuishi na za hali ya

juu pia bado ni changamoto, na uratibu usioridhisha kati ya vituo vya afya na jamii ambayo hupelekea kuwepo kwa mfumo duni wa kumsaidia mgonjwa kupata huduma na kupelekea kuwa na matokeo yasiyoridhisha ya kiafya.

Malengo ya mradi ni pamoja na:

1. Kuboresha mazingira ya kuwezesha utoaji wa huduma za afya
2. Kuboresha upatikanaji wa huduma jumuishi za afya ndani ya vituo
3. Kuongeza upatikanaji wa huduma za afya katika ngazi ya jamii

Ili kufikia malengo haya, mradi unashirikiana na Serikali ya Tanzania na washirika wengine kupanga, kutekeleza, na kusimamia utoaji wa huduma huku wakiboresha upatikanaji wa huduma za afya ya jinsia na vijana. Kwa kuongezea, mradi huu unatekelezea mifano mingi ya huduma jumuishi katika vituo vya afya na hushirikiana na jamii kuleta huduma ya afya karibu na wale wanaohitaji. Mradi huu pia unaangazia masuala kadhaa mtambuka, kama vile msaada wa lishe, kujenga uwezo, usawa, uendelevu, na kuongeza rasilimali zilizopo.

## MATOKEO

- Hadi kufikia Machi 2019, Mradi umefadhili utoaji wa huduma za afya jumuishi katika vituo 1,597 vya afya katika mikoa sita kamaifuatavyo: Kifua Kikuu (1,209), Malaria (1,199), VVU (599), Uzazi wa Mpango (1,224), na Afya ya Mama ma Mtoto (86).
- Katika robo ya pili (Januari - Machi 2019), jumla ya wateja 190,358 walipimwa VVU, ambapo asilimia 4 walipatikuwa na maambukizi. Jumla ya wateja wenye VVU 180,862 hivi sasa wako kwenye matibabu, pia kuna visa vya kifua kikuu 2,621 ambavyo vinajumuisha visa vipyaa vya maruradio ambavyo viligundulika na kutibiwa. Kwa kuongezea, asilimia 99 ya visa vyote vya Kifua kikuu vilipimwa VVU, ambapo asilimia 27 waligundulika kuwa na VVU, na asilimia 100 ya wateja wote waliotambuliwa TB / VVU walianzishiwa Tiba ya Kufubaza VVU ili kupunguza kasi ya kuenea kwa ugonjwa huo.
- Wateja 251,781 walipata angalau aina moja ya njia za kisasa za uzazi wa mpango, na wateja 2,329 walipokea huduma kwa ajili ya afya ya mama na mtoto.
- Kati ya visa 1,395,155 vilivyoshukiwa kuwa na ugonjwa wa malaria, asilimia 100 walipimwa kwa kutumia MRDT au darubini, ambapo karibu asilimia 39 walithibitika kuwa na ugonjwa wa Malaria. Kila mtu aliyethibitika kuwa na ugonjwa wa Malaria alianzishiwa matibabu kwa ajili ya tiba ya Malaria.

**BAJETI**  
\$145 million

**MUDA**  
Oktoba 2016 – Septemba 2021

**MAEneo YA MRADI**  
Iringa, Njombe, Morogoro, Lindi, Mtwara, na Ruvuma

**MBIA MTEKELEZAJI**  
Deloitte Consulting Limited

**Wabia Wengine**  
Family Health International (FHI 360), Management and Development for Health (MDH), na EngenderHealth

**MAWASILIANO YA USAID**  
Dr. Jema Bisimba  
Afisa Mwakilishi wa Mradi  
+255 22 226 684 490 X4425  
[jbisimba@usaid.gov](mailto:jbisimba@usaid.gov)

**MAWASILIANO YA MTEKELEZAJI**  
Dr. Marina Njelekela  
Mkuu wa Mradi  
+255 22 216 9000  
[mnejekela@deloitte.co.tz](mailto:mnejekela@deloitte.co.tz)

**KWA TAARIFA ZAIDI**  
Tovuti: [www.usaid.gov/tanzania](http://www.usaid.gov/tanzania)  
Facebook: USAIDTanzania  
Twitter: @USAIDTanzania